Mtenda hutendwa

Kijitabu hiki kimetayarishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza.

Waandishi:
Richard Mabala na Churchill Shakim

Mchoraji:
Daniel Mzena

Wahariri:
Justice Rutenge na Evarist Kamwaga, Twaweza

Usanifu:
Churchill Shakim

©Tamasha/Twaweza - 2013

Barua:
TAMASHA
S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania

Simu: +255-714-661-544
Baruapepe: vtamasha@gmail.com
general@tamashavijana.org
Wavuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakili nakutuma nakala mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Mara nyingine suala la maji sio rahisi kivile. Maji huweza kusababisha mgogoro kama hayatoshi. Mara nyingine pia, matumizi ya kikundi kimoja yanahatarisha maisha au ustawi wa kikundi kingine. Hali hii inaonekana wazi kwenye mto ambao unapita kwenye jamii nyingi. Iwapo jamii fulani inachafua mto kwa sababu ya kuutumia kama choo, au kunywesha wanyama wao au kufulia humohumo, jamii zinazofuata zinaweza kuathirika, hasa upande wa magonjwa. Na ni rahisi pia kwa jamii inayolalamika kuchafuliwa maji yao kusahau kwamba inachafua maji kwa wale walioko mbele zaidi. Je, ni jukumu la nani kulinda vyanzo vya maji na kuhakikisha kuwa watu wanapata maji safi na salama? Tujifunze zaidi kupitia hadithi hii.

Usisahau, ukitenda leo, utatendwa kesho.

Richard Mabala
Mkurugenzi, TAMASHA

Wahusika

Bonge
Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo
na mkereketwa wa maendeleo

Bibiye
Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati

Mwenyekiti
Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi

Mtendaji
Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe

MARUFUKU KUOGA NA KUFUA MTONI
BY UONGOZI WA KIJIJI


Hii adha ya kila siku, watu tunaugua tu matumbo.
Ni maji haya tunayokunywa. Hayafai kabisa.
ZAHANATI
Si wale wa kijiji cha juu! Wanadiriki hata kujisaidia humo-humo! Tunakunywa mikojo yao.

Tena havana haya. Halafu wanajazana kuenye zahanati yetu kutumalizia dawa.
We...dawa ni kuenda kuwaharibia na wao waone uchungu wake.
Sawasawa. Wape vidonge vyao maana Mwenyekiti wetu bure kabisa. Kazi kunyamaza tu.

Tuwachafulie na wao sasa wapate raha yake.
Tumechoka kulishwa kinyesi chao. Aaaah!
Watakoma. Kumbe mtenda hutendewa. Ala!

Nyie mnafanya nini hapa? Acheni kutuchafulia mto wetu.
Hee, kwani kuna mnayotuletea nyie hamuioni?
Ndiyooo! Mkuki kwa nguruwe... halo halooo!

Kura wehu wanatuchafulia maji makusudi. Eti wanalipiza kisasi!
Eti nini? Leo watakiona!

Kila siku mnatuchafulia maji tunaugua matumbo, sasa na nyie muone raha yake.
Unaniuaaa

Nyie mnafanya hujuma kuharibu maji.
Yote umeyataka wewe haya. Tushalalamika sana.
Sasa mwenzetu kaumizwa ndio ufurahi.

Mbona mmerudi ndoo tupu?
Ni hao majirani wametupiga.
He! lazima tulipize kisasi! Haiwezekani waumize mama zetu.



Hebu punguzeni munkari. Moto hauzimwi kwa moto.
We ndio bure kabisa. Tumelalamika mara ngapi?
Unamwogopa yule mtendaji wako. Yeye pia hawezi kazi.

Tuna kikao cha dharura cha kamati ya Ulinzi na Usalama saa tisa.
Msiongee peke yenu. Na sisi tuwemo.
Sawasawa. Chagueni vijana watatu.

Hatukubali mwenyekiti. Tumechoka kuoneiwa na wale. Lazima tulipize kisasi.
Kisasi hadi lini? Lazima kwanza tupate suluhu.
Mbona hata sisi tunachafua maji?

Je mnataka watu wa kijiji cha chini nao waanzishe vita na sisi?
Acha uzushi wako. Nataka kuwaita askari wa ulinzi kutoka wilayani.
Ili watupige sote Rungu halitatui tatizo.

Ni kweli. Ngoja niende kuongea na vijana wenzetu kule. Kisasi cha nini?
No no no, ni hatari sana.

Nifungulie, ni mimi Bonge.
Wewe unafanya nini? Huju tuko vitani? Hatari!
Itakuwa hatari kweli ukiendelea kuniacha nje kivyo? Hebu fungua bwana!

Tunataka vita kweli? Kwa nini vijana wa pande zote tusitembelee mto pamoja?
Ni kweli Bonge. Nakujua na mimi pia naweza kuwashawishi vijana wa hapa.
Basi mpango ndio huo.

Ona tangazo letu. Kweli halina maana yoyote.
Mtu akijisaidia au kufua hapa sisi tunaathirika moja kwa moja.
MARUFUKU KUOSHA NA KUFUA MTONI
BY UONGOZI WA KIJIJI

Haya sio maji ya kugombaniwa na binadamu. Heri tugombanie kuyasafisha.
Tutasafishaje?
Kwanza tusiyachafue zaidi. Tuna bahati na huu mto. Tubebe maji tufue na kujisaidia nyumbani.

Itabidi kwanza tuweke mkakati wa kulinda vyanzo vya maji pamoja na mto.
Sawa kabisa. Tukae na wongozi wa kata, twende kamati ya mto. Kisha tupewe nguvu na sheria ndogondogo.

Ona hapa miti yote imekatwa.
Muda si mrefu patakuwa jangwa.
Ni nani hao wanaolima ndani ya mto kabisa?
Ohoo, naona sasa unataka kuingilia kila kitu. Bila kulima nitaishije?
Kumbe ni wewe! Tulia bwana. Twataka kila mtu ajikimu bila kukomoa.

Watuchafulie hivihivi. Lazima wapate adhabu.
Mtendaji, tunaomba tuingie katika kamati ya mto.
Ninyi ni nani? Kamati imechaguliwa tayari.
Siku zote ilikuwawa wapi mpaka maafa yanatokea? Na bado mnagombana.

Vijana wamesema kweli.
Vijana hao wamenikumbusha mbali. Tulipokuwa vijana ilikuwa kazi yetu. Tuliheshimu nto ndio maana nao ulituheshimu.

Tukipata mfadhili, nyinyi vijana mtaweza kufanya kazi ya kusafisha mto.
Hakuna cha mfadhili tena. Ni jukumu letu wenyewe. Mabadiliko ni sisi.
Na karibu kwenye mechi ya ujirani mwema kati ya vijana.

Unaona. Ukiweka hiki kidonge kwenye maji, yanasafishika vizuri sana.
Mbona ghali?
MAJI SAFI TUMBO SAFI
GOOOOOO
Dawa ya hospitalini ghali zaidi. Bora kinga kuliko tiba.

Je wajua?

- Watu wengi, hasa watoto na wazee, wanaathirika na ugonjwa wa kuharisha na magonjwa mengine mengi yanayotokana na kunywa maji yasiyo salama.
- Hii ni kwa sababu karibu nusu ya watanzania hawapati maji kutoka vyanzo vilivyoboreshwa vilivyoko karibu na wanakoishi.
- Vyanzo vilivyoboreshwa ni kama maji ya bomba, au visima vilivyofunikwa. Ni salama kwa sababu vinazuia uchafu usiingie kwenye maji
- Hata kama chanzo cha maji ni salama, uchafu mara nyingi huingia kwenye maji wakati wa kuyachota au kuyahifadhi. Ni muhimu kusafisha maji.
- Si rahisi kusafisha mto au ziwa au kisima ambacho kimeshachafuliwa. Ni rahisi zaidi kusafisha maji nyumbani, kwa mfano kwa kuchemsha, kuweka dawa ya Water Guard na njia zingine zinazoelekezwa na wataalamu.
- Kutumia dawa na njia zingine rahisi kunapunguza sana gharama ambazo zingetumika kutibu magonjwa yanayoletwa na unywaji wa maji yasiyo salama.
- Vyama vya watumiaji maji ndio vyenye jukumu la awali la kuzuia uchafuzi wa maji. Vyama vya pamoja vitaunda Kamati za Maji za Mito na kutoa wawakilishi kwenye Bodi za Mabonde Madogo. Pamoja na kazi nyingine hizi Kamati na Bodi zina wajibu wa kutatua migogoro. Halmashauri nayo ita-shiriki kikamilifu katika Bodi za Mabonde Madogo.

Tufanyeje?

Jukumu la kulinda na kuendeleza vyanzo vya maji ni letu sote.

a) Maji ni rasilimali kwa ajili ya watu wote. Tulinde maji pamoja kwa kuunda vikundi vya watumiaji wa maji. Kama tunaishi kandokando ya mto basi tuhimize matumizi sahihi kwa faida ya wote mtoni. Tusiwaruhusu waharibifu wahatarishe maisha yetu.

b) Tuunde vyama vya watumiaji maji na kuhakikisha kwamba vinaaunda Kamati za Maji za Mito.

c) Tutumie maji yaliyo salama. Kwa pamoja tuchemshe maji au tuwahimize wenye maduka karibu yetu kuhakikisha dawa ya WaterGuard au dawa nyingine ya kufanya maji yawe safi na salama inauzwa kwenye maduka yao. Watapata faida, lakini pia watakuwa wamesaidia jamii kupambana na magonjwa.

Je, umewahi kufanya jambo lolote la kishujaa kama Bonge na Bibie?

Au unamfahamu mtu mwingine aliyefanya kitu cha kipekee kuisaidia jamii yake?

Kama jibu ni ndiyo, tungependa utusimulie!

Tafadhali tutumie hiyo stori yako iliyoleta mabadiliko hapo unapoishi au iliyotokea mahali pengine.

Tunaweza kuitumia stori yako kuandaa vijitabu au vipindi vya Televisheni na redio ili kuelimisha wengine. Usikose kutumia fursa hii!

Anuani:
Barua: Twaweza-Shujaa, S.L.P 38342, Dar es Salaam
Barua-pepe: shujaa@twaweza.org
Simu: Tuma ujumbe mfupi (SMS) bure ukijumuisha neno SHUJAA kwenda **namba 15381**